

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF WATER



WAMI-RUVU BASIN WATER BOARD (WRBWB)

WRBWB
WAMI-RUVU BASIN
WATER BOARD

REQUEST FOR EXPRESSIONS OF INTEREST
(CONSULTING SERVICES – FIRMS SELECTION)

ENHANCING CLIMATE RESILIENCE ON WATER RESOURCES IN MKONDOA CATCHMENT (ECRWRMC) PROJECT

Provision of Consultancy Services for Feasibility Assessment, Designs, Specifications, Supervision, Capacity Building and Data Integration of Hydro-Meteorological and Water Quality Monitoring Systems

Financing Agreement Reference: 5190155000109

Project ID No.: P-TZ-EAZ-004

Reference No/Tender No.: TR007/2026-2027/C/01

Date: 2nd July 2026

The Government of the United Republic of Tanzania has received financing from the African Development Bank (AfDB) toward the cost of the **Enhancing Climate Resilience of Water Resources in the Mkondoa Catchment (ECRWRMC) Project**. The project aims to strengthen climate resilience in the catchment by improving water monitoring infrastructure, enhancing early warning capabilities, integrating monitoring data into decision-making platforms, and building capacity of technical staff and community on water resource management, climate change adaptation and mitigation measures. Part of this financing will be applied to payments under the contract for **consultancy services covering feasibility assessments, preparation of designs, specifications, and tender documents, supervision of related works, capacity building of technical staff, and data integration for hydro-meteorological and water quality monitoring systems in the Mkondoa Catchment**.

The consultancy services will cover the following tasks:

a. Assessment of Existing Monitoring Infrastructure

- Conduct inventory and review of existing hydro-meteorological, groundwater, and water quality monitoring stations.
- Evaluate operational condition, spatial coverage, data quality, and integration with WRBWB forecasting systems.

b. Gap Analysis and Network Optimization

- Identify gaps and overlaps in the current monitoring network.
- Propose an optimized network design to improve spatial coverage and system efficiency.
- Design new monitoring schemes, including sites proposed in IWRM and JICA studies, using hydrological analysis, GIS, historical data review, hydraulic and water quality modeling, field reconnaissance, stakeholder consultation, and multi-criteria decision analysis (MCDA).

c. Development of Technical Designs and Specifications

- Prepare detailed designs, technical specifications, and tender documents for new and rehabilitated monitoring stations.
- Ensure compliance with Tanzania Meteorological Authority (TMA) standards, Water Resources Management Regulations (GN No. 67 of 2011), and WMO guidelines (WMO-No. 8 and WMO-No. 168).

d. Installation Supervision

- Supervise construction, installation, rehabilitation, and commissioning of monitoring infrastructure.
- Ensure compliance with approved designs, environmental standards, and quality assurance requirements.

e. Data Integration and System Enhancement

- Integrate monitoring data into WRBWB's forecasting platforms.
- Strengthen real-time data transmission, analysis, and visualization for improved early warning and decision-making.

f. Capacity Building and Knowledge Transfer

- Conduct training for WRBWB technical staff on operations, maintenance, and data utilization.
- Develop SOPs, maintenance manuals, and data management protocols for long-term sustainability.

The Wami/Ruvu Basin Water Board (WRBWB), the Implementing Agency, of this project now invites eligible consultants to express their interest in providing the above services. Interested Consultants must provide information demonstrating that they have the required qualifications and relevant experience to perform the Services (brochures, description of similar assignments, experience in similar conditions, availability of appropriate skills among staff, etc.). **Consultants may form joint ventures to enhance qualification.**

Eligibility criteria, establishment of the short-list and the selection procedure shall be in accordance with the *"Bank's Procurement Policy for Bank Group Funded Operations, dated October 2015"*, which is available on the Bank's website at <http://www.afdb.org>.

Expressions of Interest must be submitted in a written form (**hard copy** and **soft copy**) to the address below in person by **13th July, 2026 at 13:00 hrs** East African time. The submission should be clearly marked as-

"EXPRESSION OF INTEREST FOR CONSULTANCY SERVICES FOR FEASIBILITY ASSESSMENT, PREPARATION OF DESIGNS, SPECIFICATIONS AND TENDER DOCUMENTS, SUPERVISION OF RELATED WORKS, CAPACITY BUILDING AND DATA INTEGRATION IN MKONDOA CATCHMENT."

Interested Consultants may obtain further information during Office hours from 8:00 to 16.00 hours on Mondays to Fridays except on public holidays at the address below:-

The Secretary, Wami-Ruvu Basin Tender Board
30 Mazimbu Road, P.O. Box 826, Morogoro, Tanzania
Tel: 0800114031 / 0800114032 or +255 655 776 738
Email: barua@wrbwb.go.tz / pmu@wrbwb.go.tz

Basin Water Director
WAMI RUVU BASIN WATER BOARD

ORD92924

DCEA yaonya watumishi wa umma dawa za kulevya

Na Zena Chande

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imebaini kuna baadhi ya watumishi wa serikali wanaojihusisha na dawa za kulevya na kutoa onyo kuacha mara moja.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lyimo alisema katika operesheni ya Mei na Juni mwaka huu iliyofoyika nchini wamemkamata mtumishi Goodluck Nyakaselula (35) na kilogramu 106.4 za dawa za kulevya aina ya mirungi.

Lyimo alisema Nyakas-elula ambaye ni mtaalamu wa picha za kitabu katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road Dar es Salaam ni mkazi wa Mbezi Beach Dar es Salaam na alikamatwa na dawa hizo akiwa anazisafirisha kwa kutumia gari aina ya Toyota Premio lenye namba za usajili T 853 ECX.

"Huyu mtuhumiwa ni mtumishi wa serikali lakini aliomba kibali cha kwenda kusoma Nairobi, Kenya na katika masomo yake akajingiza kwenye masuala ya

dawa za kulevya na tuli-pomuhoji akasema kwamba biashara ya mirungi kuingiza Tanzania anaweza kupata fedha," alisema.

Alisema mtuhumiwa huyo ilikuwa amalize masomo yake tangu mwaka 2025 lakini kutokana na biashara hiyo akajikuta anashindwa kufanya vizuri kwenye baadhi ya masomo, hivyo kulazimika kurudia na ndipo alipoamua kusoma huku akifanya biashara hiyo.

"Kwa hiyo anasafirisha mirungi, akikutana na askari wa usalama barabarani anajitambulisha na kuonesha kitambulisho yeye ni mtumishi, kwa hiyo hakaguliwi maana anaaminika yeye ni mtumishi hawezi kusafirisha dawa lakini tumebaini na tunasubiri kumchukulia hatua za kisheria," alisema.

Alisema wapo watumishi wengine sita wamewakamata walikuwa wakisaidia usafirishaji wa dawa hizo na wanne tayari wamefikishwa mahakamani, wengine wawili wanasubiri kuchukuliwa hatua za kisheria.

Kamishna Lyimo alitoa agizo kwa askari wa usalama barabarani kumkagaua yeyote bila kujali cheo chake.

Aidha, DCEA imebaini wa-

tumishi wachache wa serikali wanatumia kumbi za starehe zenye vyumba maalumu (VIP), akitolea mfano Arusha na huko hutumia dawa hizo za kulevya.

"Kwa upande wa Dar es Salaam tumegundua wanakodisha 'apartment' (nyumba) na kufanya mambo yao huko, tutafanya msako kote huko kubaini uovu huo... Hakuna mtu anayetumia dawa za kulevya akasalimika," alisema.

Aidha, Lyimo alisema katika operesheni yao hiyo zimekamatwa tani 22.6 za dawa za kulevya, lita 30.5 na kilogramu 19.94 za dawa tiba zenye asili ya kulevya na kuteketeza ekari 228.5 za mashamba ya bangi na tani 3.3 za bangi na mirungi.

Pia, walikamata magari sita, bajaji mbili na pikipiki 33 zikihusishwa na uhalifu huo na kukamata watuhumiwa 188.

"Operesheni zilizofanyika Dar es Salaam zilifanikisha ukamataji wa kilogramu 19.94 za bidhaa zilizotambulishwa kama virutubisho vya lishe aina ya AFA CELL (Moringa Extract) katika eneo la mizigo inayosafirishwa kwenda nje ya nchi kupitia Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA)," alisema.

NGOs zahadharisha vitendo vya uvunjifu wa amani

Na Fadhili Abdallah, Kigoma

MASHIRIKA Yas- iyo ya Kiserikali (NGOs) mkoani Kigoma yameeleza kuwa uvunjifu wa amani katika baadhi ya maeneo unachangia kwa kiasi kikubwa kuchelewesha au kusitisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayolenga kuboresha maisha ya wananchi.

Mashirika hayo kupitia viongozi wake walisema hayo katika mkutano wa pamoja kujadili ushirikiano na namna ya kufanya kazi pamoja katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wananchi.

Walisema mazingira ya amani na utulivu ni msingi muhimu unaowezesha mashirika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mmoja wa wakurugenzi hao, Justine Jackson kutoka Shirika la Restless Devel-

opment Tanzania alisema migogoro na vitendo vya vurugu husababisha ugumu wa kuwafikia walengwa, kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi na wakati mwingine kusebabisha baadhi ya shughuli kusimamishwa.

Kwa upande wake, Mratibu wa miradi wa Shirika la Care Tanzania, Gidion Donalt alieleza kuwa miradi inayohusu afya, elimu, maji, kilimo, uwezesaji wa wanawake na vijana kiuchumi pamoja na huduma za kijamii zinahitaji hali ya amani na utulivu katika utekelezaji wake kinyume, hivyo hali hiyo huwanyima wananchi fursa ya kunufaika na huduma na programu zinazolenga kuinua ustawi wao.

Akizungumza katika mkutano huo, Mwakilishi kutoka Shirika la Helpage Tanzania, Francis Mkombo alisema watu wote wanapaswa kutekeleza majukumu

yao kwa kufuata katiba, sheria, taratibu na miongozo iliyowekwa na serikali.

Alisema chochote kinachopaswa kufanywa, ikiwemo kuwa na madai ni vizuri kufuata taratibu hizo na kinyume chake inakuwa chanzo cha vurugu na kuharibu amani ya nchi.

Akitoa salamu katika mkutano huo, Balozi Msaidizi wa Burundi mkoani Kigoma, Adalbert Ninahazwe alisema amani ndiyo msingi wa maendeleo kwa serikali na mashirika katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wananchi.

Ninahazwe alisema Burundi inaelewa jinsi kuvurugika kwa amani kunavyoathiri mipango ya maendeleo ambapo mashirika ya kitaifa na kimataifa hayawezi kutekeleza majukumu yao na wananchi wenye nguvu na utaalumu kama nguvukazi wanakimbia nchi kutafuta amani na mustakabali wa maisha yao ya baadaye.